



## **BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

### **ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

#### **BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI**

#### **MKUTANO WA PILI**

#### **Kikao cha Kumi – Tarehe 2 Juni, 2016.**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua zitasomwa.

#### **I. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

37. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) -  
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,  
Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mahakama Pemba inakabiliwa na uhaba wa gari kwa Majaji wanaokwenda kusikiliza kesi kisiwani humo na kulazimika kutumia gari inayokabiliwa na uchakavu kinyume na hadhi yao.

- a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka gari japo mbili kwa ajili ya Majaji wa Mahakama Kuu.
- b) Ni muda gani sasa tangu mazingira ya uhaba wa gari kujitokeza Kisiwani humo na lini tatizo hilo litaondoka.

- c) Kutokana na mazingira hayo Serikali haioni ndio chanzo cha Majaji kutokwenda kwa wakati kusikiliza kesi na kuzitolea hukumu.

**WIZARA YA ARDHI, MAJI, NISHATI NA MAZINGIRA:**

61. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Kumekuwa na kilio kwa wananchi wanyonge masikini kushindwa kumudu gharama kubwa ya kuunga umeme, ambapo hivi sasa umeme umekuwa na umuhimu zaidi kwa kuwa ni sehemu ya wananchi kujifanyia miradi ya kuongeza vipato vyao.

Je, kwanini Shirika halipeleki nguzo za umeme kama sehemu ya Miundombinu halafu mwananchi akalipia gharama za kuunga peke yake, badala ya kubebeshwa mzigo wa kulipa nguzo na uungaji ambazo ni kubwa sana.

**WIZARA YA AFYA:**

22. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ugonjwa wa kipindipindu umeingia Zanzibar tangu Oktoba mwaka jana na umeathiri baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi na baadae kuenea vijijini na watu kadhaa kuugua maradhi hayo na baadhi yao kupoteza maisha.

- a) Watu wangapi walipata maradhi ya kipindupindu na wangapi wamepoteza maisha kuanzia Oktoba mwaka jana hadi Aprili mwaka huu.
- b) Wizara kwanini inashindwa kuweka mazingira ya usafi katika masoko, maeneo ya biashara pamoja na maeneo ya makaazi ya watu kwa kutumia kanuni za afya.
- c) Sababu gani ugonjwa huu unaendelea kusambaa hadi vijijini licha ya kuwepo wataalamu wa Afya pamoja na watumishi

wanaotakiwa kutoa elimu ya Afya na kusimamia kanuni zake.

**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI:**

60. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Wananchi wamefarijika sana kwa Mji Mkongwe, kuwa hifadhi ya Kimataifa inayotambuliwa na UNESCO.

Je, wananchi wanaweza kuelezwa angalau faida kumi (10) zilizopatikana tangu Mji Mkongwe uwekwe katika hifadhi ya UNESCO.

**II. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:**

Kwamba Baraza hili liingie katika Kamati ili kujadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2016/2017.

Zanzibar,  
2 Juni, 2016.

(Raya Issa Msellem)  
**KATIBU WA BARAZA**